

Matumizi mabaya ya “Jihādi”

Kwa sababu tu kwamba neno “Jihad” linatumiwa vibaya na baadhi ya Waislamu kwa ajili ya ajenda zao za kisiasa, Waislamu hawapasi kuitelekeza dhana hii tukufu ya Imani ya dini yao. Wakati wa kuzungumzia kuhusu Jihadi, mimi nimewasikia Waislam wengi wakielezea ile Jihadi kubwa (ya kiroho) tu na kukwepa kuzungumzia hii Jihadi ndogo kwa maana ya mapambano ya silaha (kijeshi) juu ya kujihami. Sisi kama Waislam, tunasimama imara mafundisho yetu na hatuhitaji kuomba samahani kwa ajili ya hilo hata kama nyoyo au nafsi zilipotoka zitateka nyara Istilahi za Imani yetu kwa ajili ya manufaa yao ya kisiasa.

Sio watu kama Bin Laden tu ambao wanateka na kutumia vibaya Istilahi tukufu za Kiislam; tumeona vile vile hata serikali ya Marekani ikitetea hii dhana ya Jihadi ndogo pale ilipokubaliana na maslahi yake binafsi ya siasa za kidunia.

Wakati wa ukaliaji kivamizi wa Urusi huko Afghanistan katika miaka ya themanini (1980’s), Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa lilitumia mamilioni ya dola kwa ajili ya kuwagawia wanafunzi wa Afghanistani vitabu vya kiada vilivyozajwa mapicha ya vurugu na mafundisho ya “Upenda Mapambano wa Kiislamu.” Vikiwa vimechapishwa katika lugha zinazotawala za ki Afghan za Dari na Pashtu. Vitabu hivi vya kiada viliendelezwa katika miaka ya mwanzoni ya 1980 chini ya msaada juu ya ukimwi (Aids) kwa Chuo Kikuu cha Nebraska – Omaha na Kituo chake cha Mafunzo ya Afghanistan. Shirika hilo lilitumia Dola 51 milioni katika program ya elimu ya Chuo hicho ndani ya Afghanistan kuanzia 1984–1994.

Vitabu vya kwanza, ambavyo vilijazwa habari za Jihadi na kuonyesha michoro ya mabunduki, risasi, askari jeshi na mitego ya mabomu, vimetumika tangu wakati huo kama kiini cha mtaala wa mfumo wa shule wa Afghanistan. Tofauti na watoto wote duniani kote kulikobakia, ambao vitabu vyao vya kiada vya hisabati vina mapicha ya matunda ya tufaha na machungwa, watoto wa Afghanistan walifundishwa kuhesabu kwa michoro inayoonyesha vifaru, makombora na mabomu ya kutegwa ardhini.

Na kwa hiyo pale ilipofaa maslahi yake ya kimkakati, wa hila, Marekani iliendeleza utamaduni wa Jihadi miongoni mwa watoto wa Afghanistan kwenye miaka ya themanini na Raisi Reagan aliwahi hata kuwakaribisha “Mujahidina” wa Afghanistani huko White House. (Hata Taleban walitumia hivyo vitabu

vilivyotolewa na Marekani, ingawa chama hicho chenye siasa kali kulikwaruza na kufuta nyuso za binadamu katika kuendana na mfumo wao msingi halisi.) Kwa sasa kwamba ule utamaduni wa vurugu umekuja kuisumbua Marekani, utawala wa Marekani uko kinyume kabisana wazo la Jihadi na unawategemea Waislam kuiacha dhana hiyo kabisa kabisa.

Waislam hawawezi kutegemea kubadili mawazo yao juu ya dhana hii tukufu ya Jihadi, kwa sababu tu kwamba baadhi ya Waislam wapotovu au mamlaka kadhaa za kidunia wanaitumia vibaya Jihadi kama neno. Waislam wanapaswa kushutumu vikali.

Matumizi mabaya ya Jihadi na kwa kujiamini kabisa waithibitisha na kuitamka kwa dhati dhana hii ya Jihadi kama inavyoelezwa na Qur'an Tukufu na mifano mitukufu ya Mtume Muhammad (s.a.w.).

Source URL:

<https://www.al-islam.org/sw/amani-na-jihadi-katika-uislam-sayyid-muhammad-rizvi/matumizi-mabaya-ya-%E2%80%9Cjih%C3%A3di%E2%80%9D>